**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA KWA KADA ZA AFYA (MARUDIO)**

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) inawatangazia wananchi wote raia wa Tanzania wenye uwezo na sifa za kujaza nafasi za ajira za Kada za **Afya 746** kwa ajili ya Hospitali za Halmashauri, Vituo vya Afya na Zahanati watakaofanya kazi chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Tangazo hili linarudiwa kwa mara ya pili baada ya kukosa waombaji wenye sifa katika tangazo la awali lililotolewa tarehe 20 Aprili, 2022.

Nafasi zinazotangazwa ni kama ifuatavyo:-

**1. Daktari wa Meno Daraja la II – TGHS E (Nafasi 30)**

Waombaji wanatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:-

i. Wahitimu wa Shahada ya Udaktari wa Meno (Degree of Dental Surgery) kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Serikali
ii. Waliomaliza mafunzo kwa vitendo “Internship” ya muda usiopungua miezi kumi na mbili.
iii. Wenye usajili kamili (full registration) kutoka Baraza la Madaktari Tanganyika (Medical Council of Tanganyika); na
iv. Wenye Leseni hai kutoka Baraza la Madaktari Tanganyika (Medical Council of Tanganyika).

2. **Tabibu Meno Daraja la II - TGHS B (Nafasi 43)**

Waombaji wanatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:-

i. Wahitimu wa Stashahada ya Tabibu Meno (Diploma in Clinical Dentistry/NTA level 6) ya muda wa miaka mitatu kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali
ii. Wenye usajili kutoka Baraza la Madaktari Tanganyika (Medical Council of Tanganyika); na
iii. Wenye Leseni hai kutoka Baraza la Madaktari Tanganyika (Medical Council of Tanganyika).

3. **Tabibu Msaidizi - TGHS A (Nafasi 244)**

Waombaji wanatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:-

i. Wahitimu wa Astashahada ya miaka miwili ya TabibuWasaidizi (Clinical Assistant Certificate/NTA Level 5) kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali
ii. Wenye usajili kutoka Baraza la Madaktari Tanganyika (Medical Council of Tanganyika); na
iii. Wenye Leseni hai kutoka Baraza la Madaktari Tanganyika (Medical Council of Tanganyika).

4. **Afisa Mteknolojia (Maabara) Daraja la II TGHS – C (Nafasi 30)**

Waombaji wanatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:-

i. Waombaji wawe wamehitimu Shahada ya Sayansi katika fani ya Uteknolojia wa Maabara ya Afya (Bachelor Degree in Medical/Health Laboratory Sciences) kwa muda wa miaka mitatu kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.
ii. Waombaji wawe wamesajiliwa na Baraza la Wataalamu wa Maabara za Afya (Health Laboratory Practitioners' Council); na
iii. Wenye Leseni hai kutoka Baraza la Wataalamu wa Maabara za Afya (Health Laboratory Practitioners' Council).

5. **Mteknolojia (Mionzi) Daraja la II TGHS – B (Nafasi 86)**

Waombaji wanatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:-

i. Wahitimu wa Stashahada katika fani ya Mionzi (Diploma in Radiology/Radiography/NTA leve 6) kwa muda wa miaka mitatu kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

ii. Wenye usajili kutoka Baraza la Wataalamu wa Mionzi Tanzania (The Medical Radiology and Imaging Professionals Council); na

iii. Wenye Leseni hai kutoka Baraza laWataalamu wa Mionzi Tanzania (The Medical Radiology and Imaging Professionals Council).

6. **Muuguzi Daraja la II TGHS – A (Nafasi 313)**

Waombaji wanatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:-

i. Wahitimu wa Astashahada (cheti) ya miaka miwili ya Uuguzi na Ukunga (Certificate in Nursing and Midwifery/NTA leve 5) kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.

ii. Wenye usajili kutoka Baraza laUuuguzi na Ukunga Tanzania Tanzania (Tanzania Nurse and Midwifery Council); na

iii. Wenye Leseni hai kutoka Baraza la Uuuguzi na Ukunga Tanzania Tanzania (Tanzania Nurse and Midwifery Council).

**MASHARTI YA JUMLA YA WAOMBAJI WA KAZI**

i. Awe raia wa Tanzania;

ii. Awe na umri usiozidi miaka 45;

iii. Awe na vyeti kamili vya mafunzo ya fani aliyosomea (Cheti cha Kidato cha Nne, Sita, Taaluma na usajili kamili (Full Registration) na Leseni hai ya kufanya kazi ya taaluma husika);

iv. Testimonials, Provisional Results, Provisional Registration, Result Slip, Statement of Results HAVITAKUBALIWA;

v. Asiwe Mwajiriwa wa Serikali au Mwajiriwa wa Hospitali za Mashirika ya Dini ambaye mshahara wake unalipwa na Serikali;

vi. Waombaji walioajiriwa kwa mkataba wa ajira kutoka kwa Wadau wa Maendeleo katika Sekta ya Afya wanatakiwa kuambatisha nakala za

mkataba na barua za uthibitisho kutoka kwa Wakurugenzi wa Halmashauri husika;

vii. Awe hajawahi kufukuzwa, kuacha kazi au kustaafishwa katika Utumishi wa Umma;

viii. Awe na Namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIN); na

ix. Aambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa.

x. Waombaji wote waliosoma Elimu ya Sekondari nje ya nchi wanatakiwa kupata Namba ya Ulinganifu wa Matokeo (Equivalent Number) inayoanza na Herufi **EQ…** kutoka Baraza la Mitihani la Tanzania ili kuwawezesha kuingia kwenye Mfumo wa Ajira;

xi. Waombaji waliosoma Vyuo vya Nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vinafanyiwa ulinganifu/Ithibati na NACTE au TCU; na

xii. Waombaji watakaowasilisha taarifa za uongo au kughushi watachukuliwa hatua za kisheria.

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA WAOMBAJI WOTE**

i. Waombaji wote wawe tayari kufanya kazi katika Halmashauri/Vituo watakavyopangiwa;

ii. Waombaji wawe tayari kufanya kazi na Mashirika au Taasisi zilizoingiaUbia na Serikali;

iii. Baada ya kupangiwa kituo cha kazi, hakutakuwa na nafasi ya kubadilishiwa kituo cha kazi;

iv. Waombaji wote wahakikishe wanajaza taarifa zao na kuambatishanyaraka zote muhimu katika mfumo; na

v. Maombi ya ajira ni bure.

Ili kupata maelezo ya kina kuhusiana na sifa za waombaji na taratibu za utumaji wa maombi kwa nafasi za Kada za Afya, tafadhali bofya: **www.tamisemi.go.tz** auwasiliana na Kituo cha huduma kwa wateja cha Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa namba za simu **026 2160210** au **0735 160210**.

Waombaji wote wenye sifa watume maombi yao kwa njia ya mtandao kupitia kiunganishi cha ***ajira.tamisemi.go.tz.*** Waombaji waliowahi kutuma maombi yao awali kupitia mfumo wa maombi ya ajira wanatakiwa kuomba upya.

Waombaji wenye Ulemavu na sifa zilizoainishwa katika tangazo hili watume maombi yao ya kazi kwa nakala ngumu (hard copy). Maombi yao yaeleze aina ya ulemavu wao na kuambatisha picha zao na uthibitisho kutoka kwa Daktari anayefanya kazi Hospitali inayotambuliwa na Serikali. Maombi hayo yatumwe kupitia anwani ifuatayo:

Katibu Mkuu,

Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira & Wenye Ulemavu)
S.L.P.980,
**40480 DODOMA. (Aione: Mkurugenzi wa Kitengo cha Watu Wenye wdemavu)**

**Maombi yoyote yatakayowasilishwa kwa njia ya posta au kuletwa moja kwa moja Ofisini hayatafanyiwa kazi. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 02 Agosti, 2022 saa 09:30 Alasiri. Tangazo hili linapatikana katika tovuti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI ya *www.tamisemi.go.tz*.**

**Limetolewa na:** Katibu Mkuu,

Ofisi ya Rais - TAMISEMI,
Mji wa Serikali - Mtumba,
S.L.P 1923,

**41185 DODOMA.**

**20 Julai, 2022.**